



INTERNATIONAL TANFEEDS LTD

Animal Feed

Health Products

Agro Supplies

UFUGAJI BORA WA SUNGURA

SEHEMU YA TATU

UCHAGUZI WA ENEO SAHIHI KWA AJILI YA UFUGAJI WA SUNGURA.

Kwa mazingira yetu haya ya joto, unyevunyevu mkubwa na jua kali hivyo katika uchaguzi wa sehemu sahihi kwa ajili ya ufugaji wa sungura inategemeana na vitu vifuatavyo;

- Mahali maalum
- Hali ya hewa
- Mtaji
- Ukubwa wa mradi.

MAHALI MAALUM

Sehemu maalum kwa ajili ya ufugaji wa sungura ni lazima iwe inaweza kufikika kwa urahisi, iwe na miundo mbinu yote kama vile maji, barabara na umeme. Pia eneo hilo liwe na umiliki halali ili kuondoa matatizo yanayoweza kusababishwana migogoro ya umiliki wa ardhi.

HALI YA HEWA

Sehemu sahihi kwa ajili ya ufugaji wa sungura inatakiwa isiwe na joto sana, liwe eneo kavu na uwezekano wa upatikanaji wa maji kwa wingi. Pia eneo hili linatakiwa liwe na uwezo wa kuruhusu hewa ya kutosha na kuzuia upepo mkali. Hivyo napenda kushauri kuwa eneo litakalotumika liwe karibu na sehemu ambapo unaweza kupata mbogamboga kwa ajili ya kulisha sungura.

MTAJI NA UKUBWA WA MRADI.

Kiukweli kwa biashara yoyote ile ni lazima uwe na mtaji wa kutosha kwa ajili ya kujihakikishia maendeleo mazuri katika mradi wako. Hivyo kabla hujaingia katika biashara hii ya ufugaji wa sungura hakikisha umefanya upembuzi yakinifu kwa kuwashirikisha wataalam wa mifugo walioko karibu nawe ili uwe na uhakika na mradi wako. Pia kama mradi wako ni mkubwa utahitaji mtaji mkubwa pia ili kuwa na muendelezo mzuri wa mradi wako na ndio maana mtaji na ukubwa wa mradivinaendana.

JINSI YA KUBUNI NYUMBA YA SUNGURA

Kuna njia kuu mbili za kubuni nyumba ya sungura kama ifuatavyo;

1. Kuangalia jinsi wengine walivyobuni kwa kutembelea baadhi ya wafugaji wa sungura walio karibu na eneo lako ulilopanga kufugia sungura.
2. Njia ya pili ni kutumia wataalam wa mifugo waliopo karibu nawe kwa ajili ya kukusaidia kubuni ramani ya nyumba ya sungura.

MAHITAJI MUHIMU KWA AJILI YA NYUMBA YA SUNGURA

Kwa nyumba yoyote ya sungura ni lazima iwe na nafasi ya kutosha, uwezo wa kuwalinda sungura na iwe na uwezo wa kutoa mazingira mazuri kwa ajili ya ufanyaji kazi. Hivyo kabla ya ujenzi wa banda la sungura unatakiwa kuzingatia yafuatayo;

1. AINA YA SAKAFU

Sakafu inatakiwa ijengwe kwa sementi na iwe na uwezo wa kusafishika kwa urahisi. Kwa kuzingatia hayo basi sakafu inatakiwa kuwa na uwezo wa kuchukua sungura mmoja kwa mita za mraba 0.35.

0.35m² kwa sungura mmoja

2. UKUTA

Ukuta unatakiwa kuwa mrefu na wenye madirisha kwa ajili ya kuruhusu hewa kuingia ndani ya banda la sungura. Hapa unatakiwa kuwasiliana na mtaalam wa mifugo kwa ushauri zaidi.

3. AINA YA PAA LA NYUMBA

Paa la nyumba lazima liwe lina uwezo wa kuzuia majina kubwa ili kuzuia miale ya jua kuingia moja kwa moja ndani ya banda.

4. UTUNZAJI WA MAZINGIRA

Kwa banda lolote la sungura ni lazima liwe na miundo mbinu yote kwa ajili ya uondoaji taka (mbolea) na kuzipeleka mahali sahihi kwa ajili ya kutunza mazingira.

5. USALAMA

Banda la sungura linatakiwa kuwa na uwezo wa kuwalinda sungura dhidi ya majeraha, wanyama wakali (mbwa na nyoka) , jua kali, upepo mkali, makelele na wezi.

6. UWEZO WA KUSAFISHIKA KWA URAHISI.

Banda la sungura ni lazima lisafishwe kila baada ya siku 2 hadi 3 ili kuweka hali ya usafi ndani ya banda na kuweza kuzuia magonjwa ndani ya banda. Banda la sungura linatakiwa lisafishwe kwa sabuni na kemikali maalum kwa ajili ya usafi wa banda.

Ni matumaini yangu kuwa wewe mfugaji mtarajiwa hata wewe ambaye tayari umeshaanza kufuga umeweza kufaidika na kujifunza mambo mengi juu ya ufugaji wa sungura. Usikose kuungana na mwandishi wa makala hii katika sehemu ya Nne ambayo itazungumzia juu ya vifaa vinavyohitajika katika banda la sungura pamoja na lishe.

Kwa mawasiliano zaidi kuhusu masuala yote yanayohusiana na ufugaji wa sungura;

Lucas Joseph

Extension Officer ITL

0655742404/0785403023

Lucas.joseph376@gmail.com